# MAKAMBAKO YETU


www.makambakotc.go.tz | Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali | Halmashauri ya Mji Makambako


# KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI YAPONGEZA MRADI WA SOKO LA MAZAO KIUMBA KUWA MRADI NA. 1

>> Halmashauri imeweka jumla ya mil 300 za fidia, wananchi wagharamia zaidi ya Bil. 2 kujenga maghala kwa mfumo wa Jenga, Tumia,Rejesha

>> Shule ya sekondari Mbugani Kitandililo kuwa mradi na. 2 wa Halmashauri kupitiwa na Mwenge wa Uhuru 2024 (Ufunguzi wa madarasa 2 yaliyojengwa na wananchi)





# Soko la mazao la Kiumba, mradi namba moja kuzinduliwa na Mwenge wa Uhuru 2024

**Na. Lina Sanga**

Kamati ya Fedha na Uongozi ya Halmashauri ya Mji Makambako imekubali mapendekezo ya miradi itakayopitiwa na Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024,na kuagiza mradi wa soko la mazao la kiumba kuwa mradi namba moja kwani ni mradi wa Halmashauri na sio Serikali Kuu.

Kamati ya Fedha na Uongozi ilitoa rai hiyo aprili 30,2024 katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika kipindi cha kuishia robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, na kuiagiza timu ya menejimenti kuhakikisha mwenge wa Uhuru unazindua soko hilo na si vinginevyo.

Mhe.Hanana Mfikwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako alibainiha kuwa, katika Mbio za Mwenge kwa mwaka huu Halmashauri ya Mji Makambako ina miradi miwili ambayo ni soko la kiumba na madarasa mawili yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika shule ya sekondari ya Mbugani-Kitandililo miradi mingine ni ya Serikali kuu,hivyo Halmashauri inajivunia kuwa na miradi miwili ambayo itazinduliwa na kuwekwa jiwe la msingi na Mwenge, ikiwa ni miradi ambayo baraza la madiwani ilibariki utekelezaji wake.

Alisema kuwa ,Halmashauri imewekeza zaidi ya mil. 300 kwa kulipa fidia maeneo ya soko la Kiumba, na wananchi wamewekeza zaidi ya bil. 2 katika ujenzi wa maghala na vizimba , na ujenzi wa soko hilo ulifuata hatua zote kisheria ,hivyo Kamati ya fedha na Uongozi haipo radhi kupoteza fedha hizo pasipokuwa na sababu za msingi,kwani Mji unatakiwa kupangwa na kuendelezwa kwa maslahi ya Umma.

Kamati ya Fedha na Uongozi ilitoa wito kwa kamati za Mwenge za Wilaya na Mkoa kutouondoa mradi huo, na kuitaka timu ya menejimenti na TARURA kuendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya soko kama ilivyoagizwa awali.

Mwenge wa Uhuru 2024 utapokelea Halmashauri ya Mji Makambako na kukimbizwa katika Kata ya Lyamkena, Kitisi, Kitandililo na Mlowa mbapo utatembelea, kukagua na kufungua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Halmashauri .








**Na. Lina Sanga**

Wito huo ulitolewa na Mhe. Imani Fute, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha lishe na mpango wa kupunguza udumavu,katika Halmashauri ya Mji Makambako ikiwa ni kampeni ya Mkoa wa Njombe kutokomeza udumavu.

Mhe.Fute alisema kuwa, ipo haja ya wananchi kutambua lishe si jambo geni au ulaji wa vyakula vya aina fulani tofauti na vyakula vinavyopatikana kwenye maeneo yao, kwani lishe inajumuisha ulaji wa vyakula vyenye virutubisho mbalimbali ambavyo vinapatikana kwenye maeneo mbalimbali, katika Halmashauri ya Mji Makambako kama vile viazi, mahindi, mayai, maziwa, mboga za majani pamoja na matunda.

"Niwasihi wazazi kuendelea kuwalisha vyakula vyenye virutubisho watoto wenu ili kutokomeza udumavu kwani vyakula vyenye lishe ni hivi hivi vilivyopo kwenye maeneo yetu, viazi, mahindi na hata vyakula vya kibena mang'eng'e na madinyu, lakini pia nyama hata simbilisi ni nyama tuache kutafsiri lishe kwa namna tofauti",alisema Mhe.Fute.

Alitoa rai kwa wanaume kushirikiana na wake zao kipindi cha ujauzito ikiwa ni pamoja na kumsindikiza kliniki na kumsaidia majukumu mbalimbali hadi atakapojifungua na kumaliza kipindi cha unyonyeshaji.




**Na. Lina Sanga**
**Njombe**

Mpango mkakati wa miaka saba wa kutokomeza udumavu Mkoani Njombe, ulikabidhiwa kwa viongozi wa chama na makundi mbalimbali ya kijamii ili kuendeleza jitihada za utekelezaji wa Mpango huo, januari 27, 2024.

Mhe.Anthony Mtaka ,Mkuu wa Mkoa wa Njombe alikabidhi  Mpango huo kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Njombe,Mhe. Deo Sanga (MB),Viongozi wa dini,viongozi wa kimila na makundi mengine ya kijamii na kusisitiza suala la lishe kuwa agenda muhimu kwenye mikutano mbalimbali ili  kuongeza uelewa wa wananchi.

Kampeni ya lishe ya mwanao mafanikio yake, Njombe tunaweza ilipewa baraka na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa njia ya simu na kuwataka wananchi wa Mkoa wa Njombe kuendelea na kampeni hiyo ili kutokomeza udumavu katika Mkoa wa Njombe.

Kauli mbiu ya kampeni ya lishe ya mwanao mafaniko yake, Njombe tunaweza ni Kujaza tumbo si lishe,jali unachomlisha.



# Ziara ya Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa Mkoa wa Njombe, amuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako kuhakikisha machi 15,2024 wafanyabiashara wa mazao wanahamia soko la Kiumba

**Na. Lina Sanga**

Katibu wa NEC, Itikadi,Uenezi na Mafunzo CCM Taifa,Ndg. Paul Makonda februari 9,2024 alizungumza na wananchi wa Halmashauri ya Mji Makambako na maeneo ya jirani ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika Mkoa wa Njombe.

Akiwa katika Mkutano wa hadhara katika Halmashauri ya Mji Makambako,Ndg. Makonda alimuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako kuhakikisha anatekeleza maelekezo ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe kuhusu mgogoro wa wafanyabiashara wa mazao kuhamia soko rasmi la mazao la Kiumba,ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanya shughuli zao kwenye maeneo rasmi yaliyopangwa.

Makonda alitoa agizo hilo mara baada ya kupokea kero kwa wananchi ikiwa ni pamoja na mfanyabiashara wa mazao,kuhusu agizo la Mkuu wa Mkoa kuruhusu wafanyabiashara wa mazao kufanyia biashara kwenye maeneo mbalimbali badala ya soko la Kiumba na wafanyabiashara wa mali mbichi kuhamia soko la Magegele na Kiumba.

Makonda alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako,Kenneth Haule kuharakisha uboreshaji wa miundombinu katika soko la Kiumba,na ifikapo Machi 15,2024 wafanyabiashara wote wahamie soko la mazao la Kiumba.



## Watoto 16,121 wamepata chanjo ya surua katika Halmashauri ya Mji Makambako

**Na. Lina Sanga**

Halmashauri ya Mji Makambako februari 15, 2024 ilizindua kampeni ya utoaji wa chanjo ya surua rubellia, na jumla ya watoto 16,121 walipatiwa chanjo hiyo kati ya watoto 13,146 sawa na asilimia 123.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo uliofanyika katika kituo cha Afya Makambako, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, Kenneth Haule aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wenye umri chini ya miaka mitano kuhakikisha watoto wao wanapatiwa chanjo hiyo, huku akiwataka kuachana na dhana potofu dhidi ya chanjo.

Naye, Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Mji Makambako, Bi. Tindichebwa Mazara alisema kuwa, chanjo hiyo itatolewa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya na maeneo yenye mkusanyiko ili kuwafikia watoto wote.

Chanjo hiyo ilitolewa kwa siku nne mfululizo ambapo rasmi ilianza kutolewa februari 15 hadi Februari 18 ,2024 katika vituo vya kutolea huduma za Afya na maeneo yenye mikusanyiko ya watu.




**Na. Lina Sanga**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mhe.Hanana Mfikwa alitoa rai kwa wazazi kushirikiana na walimu katika malezi ya wanafunzi, kitaaluma na utunzaji wa miundombinu ya shule.

Mhe.Hanana alitoa rai februari 19, 2024 katika ziara ya kamati ya fedha na uongozi ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Kata ya Mahongole, ambapo Kamati hiyo ilifanya ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya msingi Manga.

Akizungumza na baadhi ya wazazi ambao ni wajumbe wa kamati za ujenzi wa mradi huo,aliwataka kuwa na utaratibu wa kuwashirikisha wazazi wengine juu ya umuhimu wa wazazi kushirikiana na walimu, katika malezi ya watoto wanapokuwa shuleni na hasa namna ya utunzaji wa miundombinu ya madarasa ili yatumike kwa muda mrefu.

Alisema kuwa, ipo haja kwa wazazi kufidia gharama ya kurekebisha miundombinu ya madarasa na hata madawati endapo watoto wao wameharibu, kwani kwa kufanya hivyo madarasa hayo yatatumika muda mrefu badala ya kusubiri Serikali ifanye matengenezo ambayo huenda yatachukua muda mrefu kutekelezwa.

“Niwaombe wazazi wenzangu mtoto anapovunja kioo au kuvunja dawati au kuharibu kitu chochote, gharama ijulikane na wazazi wachangie na maisha yaendelee, kwani hata nyumbani kwako ukivunja chupa ya chai unanunua nyingine kwa sababu kuna kuvunja bahati mbaya,hawa watoto wakivunja kioo wasiadhibiwe mana adhabu haifanyi kioo kuwa kizima badala yake wazazi wachangie na kuwaelimisha watoto juu ya uharibifu waliofanya”,alisema Mhe. Hanana.

Aidha,aliipongeza Kamati ya Usimamizi na  Ufuatiliaji wa miradi ya Halmashauri ya Mji Makambako,kwa usimamizi mzuri wa miradi pamoja na kamati za ujenzi za wananchi wa eneo husika kwa kujitoa katika usimamizi wa miradi hadi inapokamilika.

Kamati ya fedha na Uongozi ilitembelea miradi minne ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya Msingi Manga, Mawande, Ikwete na shule ya Msingi Makambako, shule hizo zote zilipokea fedha kiasi cha mil. 45 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili.






Madarasa mawili na ofisi moja katika shule ya msingi Ikwete (shule konge)




**Na. Lina Sanga**

Rai hiyo ilitolewa februari 21 ,2024 na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mhe. Hanana Mfikwa katika kikao na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji,Watendaji wa Kata,Mitaa,Vijiji na timu ya menejimenti ya Halmashauri ya Mji Makambako ili kuwekana sawa katika baadhi ya masuala ya kiutendaji.

Mhe.Hanana alisema kuwa,kutokana na baadhi ya sintofahamu zilizoibuka chanzo kikuu ni kukosekana kwa mawasiliano baina ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji na watendaji wa Mitaa na vijiji husika,hali iliyoibua maswali na hoja za kutoelewana katika utekelezaji wa majukumu ya kila mmoja.

Katika kikao hicho hoja mbalimbali ziliwasilishwa na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji ikiwa ni pamoja na kutopewa taarifa za utekelezaji wa masuala mbalimbali kutoka kwa Mkurugenzi,ikiwa ni pamoja kutoitishwa kwa vikao kuhusu mabadiliko ya utekelezaji wa suala la ukusanyaji wa ushuru wa taka ambao awali Mitaa ilipewa jukumu hilo.

Mhe.Hanana alitoa agizo kwa watendaji wa mitaa na Vijiji kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao,ikiwa ni pamoja na kufikisha taarifa ya masuala mbalimbali yanayofika mezani kwao,ili Wenyeviti waelewe nini kinafanyika kwenye Mitaa na Vijiji vyao ili na wao watekeleze wajibu wao kwa vyeo vyao.

Awali akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, Ndg. Kenneth

Haule alisema kuwa, kila jambo ambalo linatekelezwa kwenye Kata ,Mitaa na Vijiji ni lazima lipitie kwenye vikao vya kisheria na baada ya baraza la madiwani kubariki,  ili kutoa nafasi kwa Madiwani na Watendaji wa Kata kushusha taarifa hizo ngazi ya Kata,Mitaa na Vijiji kwa taarifa na utekelezaji wa maagizo ya Mkutano wa baraza la Madiwani.








**Na.Lina Sanga**

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Makambako machi 2, 2024 liliidhinisha rasimu ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 yenye jumla ya bil. 28.75, ambayo Halmashauri ya Mji Makambako inakusudia kukusanya kupitia vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapato ya ndani ,ruzuku kutoka Serikali kuu na fedha za nje kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

Kupitia mapato ya ndani Halmashauri ya Mji Makambako inakusudia kukusanya jumla ya bil. 4.07, ruzuku kutoka Serikali kuu bil. 21.21 na fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo bil. 3.47.

Aidha ,Halmashauri ya Mji Makambako inakusudia kutumia kiasi cha bil. 28.75 kwa kila kasma ,ambapo kiasi cha bil. 17.46 , sawa na asilimia 60.8 kwa ajili ya mishahara,bil. 3.59 sawa na asilimia 12.5 ni fedha kwa ajili ya matumizi mengine ya kiutawala na kiutendaji na bil. 7.68 sawa na asilimia 26.7 ni fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.




**Na.Lina Sanga**

Rai hiyo ilitolewa na Mhe.Imani Fute, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako katika maadhimisho ya siku ya wanawake duniani 2024, ngazi ya Halmashauri yaliyofanyika machi 6, katika uwanja vya polisi, Makambako.

Mhe.Fute alisema kuwa, wanawake wakiamua jambo wanaweza na hata katika ngazi mbalimbali za uongozi wanawake wanafanya makubwa, lakini tatizo wanawake hawapendani na huwarudisha nyuma wanawake wenzao wanapopiga hatua kwenye nyanja mbalimbali kwa sababu zisizo na mantiki.

"Wanaume hatuna shaka na uongozi wa wanawake na tunawaamini, lakini nyinyi kwa nyinyi hamuaminiani na mnavutana nyuma na mmekosa umoja", alisema Mhe.Fute.

Aidha, Mhe.Fute aliongeza kuwa, kauli mbiu ya maadhimisho hayo imekuja kwa wakati, na jamii inapaswa kuwekeza kwa wanawake ili kufikia maendeleo, kwani katika nyaja zote za maisha kama nyanja ya jamii,wanawake wamekuwa chachu katika maendeleo ya jamii na malezi ,nyanja ya Afya ambayo bila mama kuwa na Afya njema hata watoto wake hawatakuwa na Afya nzuri.

Pia aliongeza kuwa,katika nyanja ya kiuchumi wanawake wamekuwa chachu muhimu ya ukuaji wa Uchumi,kwa kujishughulisha na shughuli mbalimbali hivyo wanaume na jamii hawana budi kuwekeza kikamilifu kwa wanawake kwani wao ndiyo wanaoleta rasilimali muhimu.

Alitoa wito kwa wanawake kutojisahau katika harakati za ukombozi wa mwanamke, bali wanapaswa kutambua utamaduni kwani wajibu wa malezi ni wao,na wanaume wanapaswa kutambua

changamoto zinazowakabili wanawake kwani mwanamke si chombo cha malezi pekee  bali wawape fursa mbalimbali za kiuchumi ili kukuza pato la familia na Taifa kwa ujumla.

Mwisho aliwataka wanawake kushiriki na kugombea uongozi katika uchaguzi wa Serikali za mitaa, ili waweze kushiriki katika utoaji wa maamuzi kwani maamuzi yanaanzia ngazi za Mitaa na sio Bungeni.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani kwa mwaka 2024 ni “Wekeza kwa wanawake, kuharakisha maendeleo ya Taifa na Ustawi wa jamii”.








**Na. Lina Sanga**

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhe.Anthony Mtaka machi 8, 2024 katika sherehe za maadhimisho ya siku ya wanawake duniani, iliyofanyika Kimkoa katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe katika Kijiji cha Usita.

Mhe.Mtaka alisema kuwa , ni wakati sasa wa kufanya mabadiliko ya familia kwa kuachana na mambo ambayo wazazi wamerithishwa kwenye kitchen party za zamani, badala ya kuwafunda mabinti jinsi ya kumuhudumia mume sasa wafundishwe masuala ya kukuza uchumi na namna bora ya kuhudumia familia kwa watoto wote wa kike na kiume.

Mhe.Mtaka aliongeza kuwa, vijana wengi wa sasa hawana misingi bora ya namna ya kuanzisha familia bora,kwa kutambua majukumu ya baba na mama ndani ya familia ili kujenga familia bora yenye afya njema ,kutokana na wazazi kutowapa elimu ya malezi na familia na kuishia kuwa vijana wa hovyo wasiojitambua.

Alitoa wito kwa vijana kujifunza namna bora ya kuanzisha familia na kutambua majukumu yao ndani ya familia kabla ya kuanzisha familia, lishe ya mtoto na faida za unyonyeshaji kwa watoto kama inavyoelekezwa na wataalamu wa Afya pamoja na kuzingatia lishe ya mama mjamzito hadi atakapomwachisha mtoto kunyonya badala ya kuendelea fasheni na kutokula vyakula vyenye tija kwa afya ya mama na mtoto kwa kigezo cha kuharibu shepu na muonekano.

Aliwataka wazazi kuzingatia lishe bora kwa kuwafundisha vizuri mabinti, kuzingatia ulaji wa lishe kamili na kuwafundisha wajawazito umuhimu wa unyonyeshaji na namna ya kujihudumia baada ya kujifungua.

Pia,alitoa rai kwa wanawake kushiriki kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa,ili Halmashauri za Kijiji zote ziongozwe na wanawake na kutokujenga chuki dhidi ya wanawake wengine na kuhangaika kuwavuruga wanaofanya vizuri,kushiriki kumsema vibaya kwenye kikao badala yake wawape ushirikiano wataoshinda  uchaguzi na kuwapongeza wanapofanya vizuri.








**Na. Lina Sanga**

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, Kenneth Haule mara baada ya kutembelea kaya za wanufaika wa TASAF katika Mtaa wa Idofi,Kata ya Mlowa na kuwaagiza maafisa kilimo kuhakikisha wanaandaa ratiba ya muda wa kuweka mbolea na kupiga dawa ya wadudu kwenye miti ya parachichi ili isiathiriwe na wadudu.

Haule,alisema kuwa ratiba ikiandaliwa mapema na kuwafikia kwa wakati wanufaika hao ambao wengi wao ni wazee, itawasaidia wazee hao kuweka akiba ya fedha watakazolipwa na TASAF kwa ajili ya mbolea na dawa ili kuinusuru miti hiyo ambayo baadhi inashambuliwa na wadudu kutokana na kuchelewa kupiga dawa na kukosa mbolea.

“Miti hii ya parachichi ni fedha za Serikali ambazo zilitolewa kwa wanufaika wote ili kuwajengea uchumi endelevu baada ya miaka kadhaa,hivyo kila afisa kilimo kwenye Kata na Mitaa anawajibika kuhakikisha miti hii inakuwa na inahudumiwa ili matunda yapatikane na mnufaika apate lishe na chanzo cha mapato endelevu”,alisema Haule.

Aidha, aliwapongeza wanufaika wa TASAF kwa kuupokea mradi huo vizuri na kujitoa kuhudumia kwa ajili ya manufaa yao, kwani jitihada wanazofanya katika kuhudumia miti hiyo ni moja kati ya mafanikio ya Serikali katika harakati za kupunguza umasikini nchini.

Aidha, aliziagiza kamati za Vijiji na Mitaa zinazosimamia miradi , kuhakikisha zinasimamia vizuri miradi hiyo kuanzia ununuzi wa vifaa, mapokezi hadi malipo ya fundi , na kuzitaka kamati hizo kutoridhia malipo  endapo vifaa havina ubora au fundi kajenga chini ya kiwango hadi marekebisho yatakapofanyika.

Miradi iliyokaguliwa ni ujenzi wa madarasa 6 na matundu 12 ya vyoo katika shule ya Msingi Magomati iliyopo katika kijiji cha Usetule katika Kata ya Mahongole, ujenzi wa madarasa 3 na matundu ya vyoo 6 shule ya Msingi Ubena,Ujenzi wa nyumba pacha ya watumishi  katika zahanati ya Ikwete Katika Kata ya Lyamkena,ujenzi wa nyumba pacha ya watumishu katika zahanati ya Ngamanga katika Kata ya Utengule na nyumba pacha ya watumishi katika zahanati ya Ibatu katika Kata ya Kitandililo.







# Menejimenti ya TASAF yapongeza ushiriki na ushirikishwaji wananchi kwenye miradi ya maendeleo na uchangiaji wa asilimia kumi

**Na. Lina Sanga**

Menejimenti ya TASAF makao makuu nchini imefanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kupitia mfuko wa Maendeleo - TASAF, katika Halmashauri ya Mji Makambako na kuwapongeza wananchi kwa kushiriki katika ujenzi wa miradi kwa kuchangia asilimia 10 na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo hadi kukamilika pamoja na wanufaika wa TASAF katika Mtaa wa Idofi ambao walipewa Miche ya parachichi.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Usetule na Ibatu,Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF nchini, Ndg. Shandrack Mziray alisema kuwa maeneo mengine kuchangia asilimia 10 ni changamoto, lakini katika Halmashauri ya Mji Makambako ,wananchi wamejitoa kwa moyo mkubwa kuchangia na kushiriki hadi kukamilika kwa miradi hali inayoonyesha wananchi wana kiu ya maendeleo.

Mziray, alipongeza jitihada za uongozi wa Halmashauri ya Mji Makambako kwa kushirikisha wananchi kila hatua ya utekelezaji, ufuatiliaji na usimamizi wa miradi, na kuwapa nafasi wananchi kuimiliki miradi kwa asilimia mia moja na kuondoa maswali kati yao, kwa miradi hiyo kutekelezwa kwa uwazi hali ambayo inasaidia wananchi kutambua kiasi cha fedha za utekelezaji wa miradi na kuona namna ya kuchangia ili miradi ikamilike na kubakiwa na fedha.

Pia, aliwatoa hofu wananchi hao kuhusu maombi ya kutumia fedha zilizobaki baada ya miradi kukamilika na kuwa ahidi kuruhusu,fedha hizo kutumika kama wananchi walivyoomba ,ikiwa ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba pacha ya walimu shule ya Msingi Magomati katika Kata ya Mahongole na Uboreshaji wa miundombinu zahanati ya Ibatu katika Kata ya Kitandililo pamoja na ujenzi wa jiko la nje nyumba ya watumishi katika zahanati hiyo.

JARIDA LA ROBO JANUARI MACHI.indd 19 5/24/2024 12:32:43 PM

Timu ya menejimenti ya TASAF ilitembelea na kukagua miradi mitatu ambayo ni ujenzi wa madarasa 6 na matundu 12 ya vyoo shule ya msingi Magomati katika Kijiji cha Usetule, Kata ya Mahongole na Ujenzi wa nyumba pacha ya watumishi zahanati ya Ibatu katika kijiji cha Ibatu,Kata ya Kitandililo na mradi wa parachichi kwa wanufaika wa TASAF katika Mtaa wa Idofi,Kata ya Mlowa.








**Na. Lina Sanga**

Sekta zinazotoa huduma kwa jamii zimetakiwa kushirikiana katika kupanga matumizi ya ardhi kuepusha migogolo na wananchi.

Rai hiyo ilitolewa na Mhe. Imani Fute, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako katika mkutano wa baraza la Madiwani la kuishia kipindi cha robo ya tatu (januari -machi) 2023/2024, uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri mei 7, 2024.

Mhe.Fute alisema kuwa, ipo haja kwa mamlaka zote zinazohusika na utoaji wa huduma kwa wananchi, kama mamlaka za huduma ya maji, barabara na umeme na idara ya ardhi na mipango miji, kushirikiana pamoja katika upimaji na upangaji wa ardhi,ili ijulikane matumizi ya viwanja kwa kubainisha wapi itapita barabara,uwekaji wa miundombinu ya umeme na huduma zingine kabla ya mwananchi kufanya ujenzi.

Aidha, alitoa rai kwa Mkurugenzi na timu ya menejimenti kulichakata suala la ujenzi wa shule ya sekondari ya Kata ya Mwembetogwa, baada ya Serikali kujenga shule mpya ya Azimio kupitia mradi wa BOOST na eneo la awali kubaki na majengo chakavu.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Kipolisi Makambako, OCD Omary Diwani alitoa rai kwa jamii kushiriki katika kuzuia uhalifu na uvunjifu wa amani, badala ya kulitegemea jeshi la polisi pekee, na kusisitiza jamii kuachana na imani potofu kwani kifo kipo na kila mmoja atakufa.

JARIDA LA ROBO JANUARI MACHI.indd 21 5/24/2024 12:32:44 PM

## Matukio yajayo......






JARIDA LA ROBO JANUARI MACHI.indd 23 5/24/2024 12:32:44 PM




**Jarida hili limeandaliwa na;**
**Kitengo cha mawasiliano ya Serikali**
**Halmashauri ya Mji makamba**
**Mei 24, 2024**